

JINSI PROGRAMU/KIPENGELE CHA WA NOTIFY HUFANYA KAZI

Washington Exposure Notifications (WA Notify) ni zana muhimu ya kusaidia kukomesha kuenea kwa COVID-19. Kama vile kuvaa barakoa, kudumisha umbali kati yako na wengine na kupata chanjo, WA Notify ni njia nzuri ya kulinda jumuiya yetu.

Programu/kipengele cha WA Notify hufanya kazi kuitia simu mahiri, bila kushiriki maelezo yoyote ya binafsi, ili kuwaarifu watumiaji iwapo huenda wamekaribiana na mtu aliyeambukizwa COVID-19. **Ni zana ya faragha kabisa na haikutambui wala kufuatilia utambulisho wako au mahali unapoenda.**

Tafiti zimetambua kuwa kadri watu wengi wanavyozidi kutumia arifa za kukaribiana na aliyeambukizwa, ndivyo manufaa yanavyozidi kuwa makubwa. Mifano ya data katika jimbo la Washington inaonyesha kuwa hata kama idadi ndogo ya watu watatumia programu/kipengele cha WA Notify, hatua hii itapunguza maambukizi na vifo.

KUWEKA PROGRAMU/KIPENGELE CHA WA NOTIFY KWENYE SIMU YAKO

Kwenye simu yako ya iPhone:

1. Nenda katika Mipangilio
2. Sogea chini hadi kwenye sehemu ya Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa
3. Bofya "Washa Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa"
4. Chagua Marekani
5. Chagua Washington

Kwenye simu yako ya Android:

1. Nenda kwenye programu ya [Duka la Google Play](#)
2. Tafuta Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa za WA (WA Exposure Notifications) ili upate programu kwa urahisi
3. Pakua programu ya Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa katika Washington



BAADA YA KUWEKA PROGRAMU/KIPENGELE CHA WA NOTIFY KWENYE SIMU YAKO

Ifuatavyo ndivyo jinsi programu hufanya kazi ili kusaidia kuzuia kusambazwa kwa COVID-19.




Watu wawili wanaotumia WA Notify kwenye simu zao mahiri wanapokuwa wamekaribiana, simu zao hubadilishana misimbo nasibu kwa kutumia Bluetooth. **Misimbo haitambuliki kabisa na haifuatili mahali mtu alipo au kubadilishana taarifa binafsi.**



Kutokuwa na habari ni habari njema. Mtu akipatikana kuwa na COVID-19 kuitia kipimo kilichothibitishwa na maabara, afya ya umma itamatumia ujumbe wa maandishi wa kiungo cha uthibitishaji na/au arifa ibukizi. Vinginevyo, mtumiaji anaweza kuomba msimbo wa uthibitishaji kwa ajili ya matokeo chanya ya kipimo cha nyumbani.



Kisha mtu aliyepatikana kuwa ameambukizwa COVID-19 **atabofya kiungo** au arifa na **kufuata hatua zote** ili kuthibitisha matokeo yake kwenye ptogramu.



Watumiaji wa WA Arifa hupokea arifa kwamba wanaweza kuwa wamekaribiana na mtu aliyeambukizwa COVID-19 ikiwa walikuwa karibu na kuwa na uwezekano wa kuambukizwa na **mtumiaji asiyejulikana wa WA Notify ambaye alipimwa na kupatikana kuambukizwa COVID-19 hivi majuzi.**



Arifa zina kiungo cha kuelekeza kwa taarifa kuhusu hatua inayofuata unayopaswa kuchukua ili kujilinda na kuwalinda watu wengine. **Hazina taarifa yoyote kuhusu mtu aliyepatikana kuwa ameambukizwa COVID-19 wala mahali ambapo huenda ulikaribiana na mtu aliyeambukizwa COVID-19.**